# Wafugaji watakiwa kuondoa mifugo shamba la miti Mtibwa

**Na MWANDISHI WETU, *MVOMERO***

SHAMBA la miti Mtibwa lililopo Pagale, wilayani Mvomero mkoani Morogoro, linakabiliwa na changamoto ya wafugaji kuvamia kambi za wahifadhi.

Hayo yamebainika wakati Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ilipotembelea shamba hilo linalomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) hivi karibuni, kufanya ukaguzi wa kazi zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za ruzuku ya zaidi ya sh. milioni 500 iliyotolewa na TaFF kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2021.

Kamshina Mhifadhi Mkuu wa Misitu (TFS), Profesa Dos Santos Silayo alisema changamoto kubwa kwa shamba hilo ni wafugaji kuchunga katika maeneo ya hifadhi au kupitisha mifugo yao na baadhi ya hawana makazi katika vijiji vya jirani, hivyo wanalazimisha kubaki katika eneo la msitu jambo ambalo halikubaliki.

"Nitoe wito kuendelea kuisimamia rasilimali hii, nashukuru kwa askari waliopo katika eneo hii wanafanya kazi vizuri. Mwenyekiti na Bodi yako naomba muendelee kusaidia shamba hili katika kutekeleza hadhi yake na kazi kubwa ni kuhakikisha hakuna uharibifu wa kile ambacho tumekifadhili,"alisema Profesa Dos Santos.

Awali Mhifadhi Msaidizi wa Shamba la Miti Mtibwa, Karimo Mangachi alisema ndani ya siku nne wamekamata ng'ombe 900 katika eneo la ndani la kilomita tatu.

"Tangu mwezi wa kwanza hadi leo kumekuwa na matukio ya kuvamiwa zaidi ya kumi, changamoto hii imekuwa ni tishio kwa wenzetu tuliowapa jukumu la ulinzi ambao ni Suma JKT wanaonekana kuzidiwa nguvu,"alisema Mangachi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Misitu Tanzania, Profesa Romanus Ishengoma alisema TFS ni Jeshi Usu na utaratibu wa kulinda katika kukabiliana na tatizo hilo.

Katibu Tawala wa Mfuko wa Misitu, Dk. Tuli Msuya aliwapongeza viongozi wa shamba hilo kwa jitihada zao kubwa za kupambana na changamoto hizo na kuwataka kuendelea kuitunza miti iliyopandwa katika eneo hilo.

Uhuru Uk.16, Tarehe 16/06/2021

Scanned with CamScanner

# Lake Zone fishermen receive huge boost from IRDP, UNDP

**By Correspondent Valentine Oforo,**

**Dodoma**

THE Institute of Rural Development Planning (IRDP) has installed a modern cold room and ice flake production machines in Mwanza Region in a robust project aimed to improve business performance among fishermen in the lake zone.

Dubbed Kibala Cold Room and Ice Flake Processing Industry, the state-of-the-art plant which had received lucrative financial patronage from United Nations Development Programme (UNDP) targets to enable the fishermen executing their trade at advance levels and thus, fetching international markets.

Briefing The Guardian over the vital economic investment, Senior Lecturer and Project Coordinator at the Institute, Bonamax Mbasa, detailed that the state-owned varsity had decided to venture into the project after realising that the fishermen in Lake Zone were failing to attract international markets due to poor technology.

"With the facility, the fishermen at the lake zone are currently able to professionally conserve their catches for at least three days before being exported to the far outside markets," he said.

He added: "With the so far installed factory, the fishes from the lake zone are now reaching the far markets at recommended fresh condition, the situation which was not the case before."

He insisted that the vision of the Institute was to continue powering more youth to realise and venture into numerous economic opportunities that the country has been endowed with.

"Among out role is to also research over different challenges that upset the entrepreneur youth and women and thus, assisting them through implementation of relevant projects," he stated, added, "For instance, IRDP is the sole high learning institution which embrace Competence Based Education Training System (CBETS), the system which focuses to impart the students with knowledge and skills with an eye to change their altitude."

21631200l

The Guardian pg.6, Tarehe 16/06/2021

Scanned with CamScanner